Cadnidate's name/ Index number …………………………………………………………

**THE PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**BUNDA DISTRICT COUNCIL**
**FORM TWO PRE-NATIONAL ASSESSMENT**
**021 KISWAHILI**

**Time: 2½ hours** **Septemba 2023**

---

**Maelekezo**

1. Mtihani huu una sehemu tatu A, B, na C.
2. Jibu maswali yote.
3. Fuata maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Zingatia unadhifu wa kazi.

wazaelimu.com

**SEHEMU A (Alama 15)**

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x) kisha andika herufi ya jibu hili katika kisanduku kilicho mbele ya swali.

(i) Katika neno amefiwa, mzizi wa neno hilo ni
A. a
B. me
C. fi
D. efi
E.f

(ii) Bwana atakaporudi tutamlaki mawinguni. Hii ni aina gani ya rejesta?
A. Hospitali
B. Mtaani
C. Shambani
D. Kanisani
E. Hotelini

(iii) Upi ni uchanganuzi sahihi wa mofu zinazounda kitenzi vimeshabihiana. A. Vi-me-sha-bi-hi-a-na.D. Vi-me-shabihian-a
B. Vi-me-sh-bi-hi-an-a E. Vime-shabi-hi-an-a.
C. Vi-me-sha-bi-hi-an-a

(iv) Ni mambo gani muhimu ya kuzingatia katika kuteua maneno na miundo ya tungo wakati wa mazungumzo?
A. mada, muktadha na uhusiano baina ya wazungumzaji
B. mada, mazungumzo na uhusiano wa wazungumzaji
C. mada, mzungumzaji na muktadha na mazungumzo
D. mada, mzungumzaji na uhusiano wa wazungumzaji
E. mada, muktadha na mazungumzo

(v) Ipi kati ya sentensi zifuatazo ina kiambishi cha urejeshi nafsi ya pili umoja? A. wao walituibia nguo zetu D. Nimekiona kilichopotea
B. Baba anamuonea huruma E. wewe umemuona toka mbali
C. nitakununulia nguo mpya

(vi) Ipi kati ya seti zifuatazo ni seti ya mambo yaundayo fasili ya lugha.
A. kukidhi hoja ya mawasiliano , sauti, nasibu, maana, kukosoa jamii
B. sauti, nasibu, kukubaliwa na jamii, kukidhi haja ya mawasiliano

C. mofimu,sauti, nasibu, maana, kukubaliwa na jamii, kukidhi haja za mawasiliano
D. sauti, nasibu, maana , kukubaliwa na jamii , kuelimisha E. sauti, maana , nasibu, fonimu , kukubaliwa na jamii.

(vii) Sababu mojawapo ya utata katika lugha ya mazungumzo ni ipi kati ya zifuatazo:
A. Kutokuzingatia sarufi na mantiki.
B. kutotumia neno lenye maana zaidi yamoja
C. kutotumia kiwakilishi kiambata
D. kutoweka msisitizo au ufafanuzi zaidi
E. kutumia mofimu sahihi za wakati

(viii) Katika neno "Fung**u**a" kiambishi kilichokolezwa wino kina dhima gani?
A. Kauli ya
B. Kauli ya kutendua
C. Kauli ya kutendeka
D. Kauli ya kutenda
E. Kauli ya kutendeana

(ix) Tarakimu za kipeuo zinazotumika katika kamusi kuwa na dhima ipi?
A. kufupisha maneno
B. Kuonesha vidahizo ambavyo ni homonimu.
C. ketenga maana ya maneno
D. kuonesha vipeuo vya hesabu
E. kuipamba kamusi

(x). Tungo za kifasihi na zile zisizo za kifasihi hutofautiana hasa katika ……
A.Waandishi B. Wasomaji.C. Wasimuliaji.D.Muda
E. Lugha inayotumika.

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

2. Oanisha dhana zilizopo fungu A na mifano yake iliyopo fungu B kwa kujaza herufi ya jibu sahihi kwenye fungu A

| Fungu A | Fungu B |
|---|---|
| (i) Mvua za rasharasha<br>(ii) Kale kakuku kadogo keupe kako kwako kaka?<br>(iii) Pambana na hali yako<br>(iv) Miti yote nitapanda ila mtarawanda utanishinda.<br>(v) Eee mwanangu kuwa vema huko huko tumboni ukijua ya kuwa mimi mama yako ninakupenda sana tena zaidi ya sana! | A. Msemo<br>B. Nahau<br>C. Simo<br>D. Fumbo<br>E. Mzungu<br>F. Ritifaa<br>G. Lakabu<br>H. Kitanzandimi.<br>I. Methali.<br>J. Kitendawili. |

| i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

**SEHEMU B (Alama 70)**

3. Tunga sentensi kwa kutumia aina zifuatazo za maneno
   (a) **Za Tanga** litumike kama kiwakilishi cha a-unganifu
   (b) **U** litumike kama kitenzi kishirikishi
   (c) **Kazini** litumike kama nomino.
   (d) **Ndege** litumike kama nomino ya kawaida.
   (e) **Vizuri** litumike kama kivumishi cha sifa.

4. Eleza maana ya Istilahi zifuatazo kwa mfano
   (i) Fonimu -------------------------------------------------------------------------------------
   (ii) Unominishaji ------------------------------------------------------------------------------
   (iii) Kidatu-----------------------------------------------------------------------------------
   (iv) Kiimbo------------------------------------------------------------------------------------
   (v) Kamusi mahuluti---------------------------------------------------------------------------

5. Chunguza sentensi zifuatazo , kisha bainisha chanzo cha utata wa sentensi hizo.
   (a) Dada anampenda mama kuliko mimi
   (b) Rose ametumwa na Daudi
   (c) Dismas amelalia uji
   (d) Mwalimu Hamisi atafika kesho
   (e) Bokobora ameondoka nyumbani

6. Fasihi simulizi ni utanzu wa fasihi wenye mambo anuai. Ili fasihi simulizi iweze kuwasilishwa inahitaji mambo makuu matano. Yataje na uyaelezee.
7. Kitendawili ni kipera cha fasihi simulizi kinachosaidia kukuza udadisi kwa jamii. Onesha sehemu tano za kitendawili kwa mifano.
8. Taja njia iliyotumika kuunda misimu ifuatayo:
   (a) Pamoko (Pamoja) ____________________________________________________
   (b) Mataputapu (pombe ya kienyeji) ________________________________________
   (c) Denti (Mwanafunzi) _________________________________________________
   (d) Unga wa Yanga (Unga wa njano) ________________________________________
   (e) Utajiju (Utajijua) ____________________________________________________
9. Hakiki shairi lifuatalo kwa kuzingatia mwongozo wa maswali yanayofuata chini yake.

Ufataki waenea, na kuzidi hapa kwetu,
Ulaya umetokea, huko umeshika kutu,
Matokeoye twajua, fedha yawa ndiyo kitu,
Mijini hata Pwani, ufataki umezidi.

Nitaeleza bayana, fataki ifahamike,
Mzee kupenda sana, wale watoto wa kike,
Marika kutoringana, maana hii mushike,
Mzee anazuzuka, huyu awa mfataki.

Ni maradhi ya utosi, wazee yamewakaa,
Uzee wanauasi, japo mvi zimewajaa. Uzee
waona tusi, unawanyima vifaa, Shikamoo
ukiwapa, wanaikwepa marahaba.

Waitwa mashughadadi, wazungu wametamka,
Sukari wanainadi, watoto wanaisaka, Fedha
yafanywa waridi, vimwana vyasisimka,
Vijana wadhulumiwa, ndiyo mfumo wa fedha.

Na mfataki wa kike, hutokea aghalabu,
Madaha yake ya kike, kijana mwenye adabu,
Kuoa asikumbuke, ati ndoa ni sulubu,
Kijana awekwa ndani, tadhani kapewa
dawa.

Wakaitwa shugamami, nao fedha wazimwaga,
Manukato yawahami, ya ujana kuyaaga,
Wazo laleta kichomi, kijana afanywa shoga, Ufataki
ni tama, tama isofikiri.

**<u>Maswali</u>**

i) Bainisha kichwa cha shairi hili
ii) Je, mtunzi wa shairi hili ametumia mtindo gani? Eleza
iii) Hakiki muundo wa shairi hili.
iv) Wewe ukiwa kama kijana umejifunza nini kutokana na shairi hili?
v)Bainisha vipengele viwili vya matumizi ya lugha vilivyotumika kwenye shairi hili

**SEHEMU C ( Alama 15)**

10. Kampuni ya Vodacom imetangaza nafasi tatu za ajira katika idara ya uhasibu kupitia gazeti la Nipashe la tarehe 20/04/2022 Watu wote wenye sifa stahiki wanatakiwa watume maombi yao kabla ya tarehe 20/09/2022 kwa mkurugenzi mkuu wa Vodacom, S.L.P 34028 Pwani. Hivyo mwandikie barua Rafiki yako ukimjuza kuhusiana na fursa hizo.Jina lako liwe, NAKIPENDA KISWAHILI.